

Mambo ya Msingi ya Sandata Mobile Connect ya Electronic Visit Verification (Uthibitishaji wa Ziara ya Kielektroniki)

(Electronic Visit Verification Sandata Mobile Connect Essentials)



Februari 2024

P-02751SW (03/2024)

Karibu kwenye Department of Health Services (Idara ya Huduma za Afya) ya Wisconsin, Mambo ya msingi ya EVV. Kila unachotakiwa kujua kuhusu programu ya Sandata Mobile Connect—pia inayojulikana kama programu ya SMC.

Ikiwa wewe ni mgeni kwenye wakala wako—mgeni kwenye EVV—ikiwa ungependa kujifunza zaidi kuhusu mambo ya nje na ya ndani ya programu ya SMC, kipindi hiki ni chako! Leo, tunashughulikia kila kitu unachohitaji kujua kuhusu programu ya SMC

Ajenda

- Tathmini vipengele vipya vya programu ya Sandata Mobile Connect (SMC).
- Kujifunza jinsi ya kuingia na kukamilisha ziara kwenye programu mpya ya Sandata.
- Kujifunza jinsi ya kuweka upya nenosiri la programu ya SMC
- Kujifunza vidokezo muhimu na mahali pa kupata rasilimali.



2

Kipindi cha leo kimejitolea kushiriki kila tunachojua kuhusu programu ya SMC. Ikiwa wakala wako hautumii mfumo wa EVV wa Sandata uliotolewa na Jimbo, mafunzo haya hayatakuwa ya msaada kwako. Pia ikiwa hutumii mfumo uliotolewa na Jimbo, tunapendekeza kuwasiliana na muuzaji wako mbadala wa EVV kwa usaidizi.

Baadhi ya vipengee tutakavyoshughulikia katika kipindi hiki:

Kuhakiki vipengele vipya vinavyokuja

Kujifunza jinsi ya kuingia na kukamilisha ziara kwa kutumia toleo jipya la programu hii—hata wakati ambapo hakuna Wi-Fi yoyote au simu yoyote inayopatikana. Tunapendekeza kutumia programu mpya; nembo yake imeonyeshwa hapa.

Kujifunza jinsi ya kubadilisha nenosiri la programu yako ya SMC—moja kwa moja kwenye kifaa chako.

Tutashiriki vidokezo tunapoendelea kwa kutumia programu ya SMC na mahali pa kupata rasilimali za EVV za kusaidia.

Kumbuka - Nembo unayoona kwenye sehemu ya chini ya slaidi hii ni programu tunayozungumzia leo. Hakikisha unatumia toleo hili la programu.

Maneno ya Kawaida

- **Electronic Visit Verification (Uthibitishaji wa ziara ya kielektroniki) (EVV)**— Mfumo unaotumia teknonolojia kuthibitisha kuwa huduma zilizoithinishwa zilitolewa (Wafanyakazi wanapaswa kutuma maelezo mwanzoni na mwishoni mwa kila ziara.)
- **Programu ya SMC**—Kifaa kinachotumiwa na wafanyakazi kuingia na kutoka kwenye ziara
- **Sandata EVV Portal (Ukurasa wa EVV wa Sandata)**—Kifaa cha kiusimamizi cha kuthibitisha alama za data za ziara kuu

3

Kwenye skrini utaona baadhi ya maneno ya kawaida yatakayotumiwa katika mafunzo yote ya leo na ndani ya mfumo wa Sandata.

1 Electroic Visit Verification (Uthibitishaji wa ziara ya kielektroniki) (EVV) ni hitaji la shirikisho la kunasa maelezo ya ziara kielektroniki.

2 Programu ya Sandata Mobile Connect (SMC) ndio njia ya haraka zaidi ya kunasa ziara yako kwa wakati wa kuingia na wakati wa kutoka.

Unapoendeleza huduma zinazohitaji EVV, wafanyakazi huingia kwenye programu ya SMC mwanzoni na mwishoni mwa ziara. Programu ya SMC hukusanya maelezo yanayohitajika—rahisi!

3 Sandata EVV Portal (Ukurasa wa EVT wa Sandata) ni kifaa cha kiusimamizi. Watoaji huduma hutumia kifaa hiki kuhakikisha kuwa maelezo yote ni sahihi kwa ajili ya ziara.

Maneno ya Kawaida

- Mteja—mwanachama au mshiriki ambaye anapata huduma kupitia mpango wa Medicaid
- Mwajiriwa—Mtu (mfanyakazi) ambaye hutoa huduma kwa mteja mmoja au zaidi
- Kitambulisho cha Kampuni—Nambari ya utambulisho ya wakala katika Sandata

4

Mwishowe:

4 Mteja **ni mwanachama** au mshiriki ambaye hupokea huduma kupitia Wisconsin Medicaid.

5 Mfanyakazi **ni mtu** au mwajiriwa anayetoa hutunzaji kwa mteja.

6 Kitambulisho **cha kampuni** ni nambari ya utambulisho ya wakala na hutumika katika mchakato wa kuingia kwa programu ya SMC. Tutajifunza mahali pa kupata nambari hii baadaye katika mafunzo haya.

Hebu tuzungumze kidogo kuhusu kile ambacho EVV ya data hukusanya.

Data ya EVV Inayohitajika na Shirikisho



5

EVV ni mfumo unaotumia teknolojia kurekodi tarehe na mahali ambapo mfanyakazi hutoa huduma kwa mtu binafsi mwanzoni na mwishoni mwa kila ziara.

Hizi ni Pointi sita Kuu za Data zinazonaswa. Tutaanza kwenye safu ya kushoto

EVV hutumia teknolojia kurekodi:

1. **Ni nani** anayepokea huduma
2. **Ni nani** anayetoa huduma hiyo
3. **Ni** huduma gani inayotolewa
4. **Pale** ambapo huduma hutolewa
5. **Tarehe** ya huduma
6. Pamoja na **wakati wa kuingia** na **wakati wa kutoka**

Tafadhali kumbuka: EVV sio mfumo unaofuatilia eneo katika wakati wote wa ziara. Eneo unaswa tu mwanzoni na mwishoni mwa ziara. Hakuna kinachokusanywa huku ziara inapoendelea.

Pata Programu ya SMC



WISCONSIN DEPARTMENT
of HEALTH SERVICES

Programu ya SMC

- Programu ya SMC inapatikana kwenye vifaa vya Android na Apple.
- Ni upakuzi bila malipo kutoka kwa Apple Store na Google Play.
- Tafuta "Sandata Mobile Connect" na utafute nembo hii:



7

Sandata imesasisha programu yao. Hii hapa ni picha ya matoleo yote mawili ya programu ya SMC.

Toleo la zamani lina nembo yenye mandharinyuma ya rangi nyeupe na mshale wa rangi ya dhahabu. Usipakue au kutumia toleo hili Halitasasishwa. Huku muda unavyosonga, huenda ukapata utendakazi wa programu hii ukififia.

DHS inapendekeza ubadilishe kwenye programu mpya ya SMC, iliyo na mandharinyuma ya buluu nyeusi.

Kwa wale wanaotumia programu kwa sasa, ni wangapi wanaotumia toleo la buluu nyeusi? Tafadhali inua mkono yako mtandaoni.

Unaweza kutafuta katika Google Play (kwa watumiaji wa Android) au App Store (kwa watumiaji wa iPhone) kwa "Sandata Mobile Connect," tafuta aikoni mpya, ana uipakue.

Utaombwa kuweka upya nenosiri lako. Nenosiri hili mpya litatumika kwa wakala wowote ambao ni mtoa huduma unayemfanyia kazi anayetumia Sandata. Hiki ni kipengele kipya ambacho kitakuwa cha msaada kwa wale miongoni mwenu wanaofanyia kazi mtoa huduma zaidi ya mmoja.

Jisikie huru kufuta toleo la zamani la programu hii, aikoni ya rangi nyeupe, mara utakapopakua toleo jipya.

Leo tutakuwa tukiangazia toleo jipya tu la SMC. Tunapendekeza matumizi yake.

Kidokezo cha Mafunzo: Leo, pale ambapo unaona eneo la kujaza au kitufe cha kubofya kwenye picha za skrini za programu yetu, ipe akili yako jinsi ya kukumbuka. Tumia kidole chako na uguse sehemu hiyo ya slaidi, kana kwamba ni simu au kompyuta yako kibao. Hii huunganisha akili yako kwenye misuli yako kwa ukumbukaji bora zaidi.

Nitawapa nyote dakika moja ya kugusa nembo mpya ya Sandata kwenye skrini. Chagua nembo hiyo ya programu mpya na hebu tuendele.

Muhtasari wa Mabadiliko ya SMC

Vipengele vipya vilivyo sasa katika programu ya SMC:


- Maelezo ya mtoa huduma ya kiotomatiki
- Nenosiri moja kwa akaunti zote za mtoa huduma
- Kuweka upya nenosiri kwa urahisi
- Modi ya nje ya mtandao iliyo ya kawaida zaidi
- Uchaguzi wa nyumbani/jamii
- Chaguo la kubadilisha huduma
- Misimbo ya huduma za ziada
- Siku saba za ziara za awali
- Chaguo la mteja la maelekezo/simu



Ingia kwenye Programu ya SMC

Ilani ya SMC

- Sandata itatuma barua pepe kwa mfanyakazi yenye nenosiri la muda mfupi na Kitambulisho cha Kampuni.
- Barua pepe sawa inaweza kutumika kwa mawakala mengi.



10

Kwa wafanyakazi wapya kabisa, ikiwa ni pamoja na wauguzi wa kujitegemea walio wageni kwa EVV: Haya hapa ni maelezo kuhusu unavyofikia programu ya Sandata.

Mtoa huduma wako anaweka maelezo ya wafanyakazi wake katika Wisconsin's ForwardHealth Portal (Tovuti la ForwardHealth wa Wisconsin) na yanatumwa kwenye Sandata. Ikiwa wewe ni muuguzi wa kujitegemea, lazima uongeze taarifa yako kwenye ForwardHealth Portal (Tovuti la ForwardHealth) mwenyewe. Sandata inatuma barua pepe kwa kila mafanyakazi.

Mara unapopokea barua pepe yako ya mwaliko kutoka kwa Sandata iliyo na jina lako la mtumiaji (ambalo ni anwani yako ya barua pepe; hapa, iko kwenye eneo lenye rangi ya buluu yenye uluwiluwi) na nenosiri la muda mfupi, uko tayari kuingia!

Ikiwa hujapokea barua pepe yako ya mwaliko kutoka kwa Sandata, tazama kwenye kichujio cha barua taka cha barua pepe yako. Unaweza pia kutumia kipengele cha utafutaji cha barua pepe yako kutafuta neno, "Sandata." Ikiwa hujapokea barua pepe hii ya awali, mjulishe msimamizi wako wa shirikia kwamba bado unahitaji kuongezwa kwenye EVV.

Wauguzi wa kujitegemea, habari ni: Utapata ufikiaji wa sehemu mbili za mfumo wa Sandata kwa majukumu yako mawili:
Sandata EVV Portal (Tovuti ya Sandata EVV): kwa jukumu lako la kiutawala
Programu ya Sandata Mobile Connect, iliyoonyeshwa hapa, kwa jukumu lako la mfanyakazi
Kuwa makini kwa barua pepe na manenosiri yako kwa kila sehemu ya mfumo.

Huduma ya Wateja ya EVV wanaweza kujibu maswali ambayo wewe au msimamizi wako wa shirika mnaweza kuwa nayo. Tutashiriki maelezo zaidi kuhusu Huduma ya Wateja baada ya muda mfupi.

Unapaswa kuwa mtu wa pekee anayetumia barua pepe hiyo, kwani itakuwa jina lako la mtumiaji katika Sandata. Iwapo unafanya kazi kwa wakala zaidi ya mmoja, unaweza kutumia anwani sawa ya barua pepe kwa kila wakala.

Hapo awali, ungehitaji manenosiri tofauti kwa kila wakala uliolifanyia kazi. Hii kamwe haihitajiki tena! Nenosiri lilelile la Sandata litatumika kwa kila wakala kwa ajili ya mfanyakazi.

Kitambulisho cha Mfanyakazi wa EVV



Wisconsin Electronic Visit Verification
WORKER VISIT CARD
 Wisconsin EVV Customer Care
 833-931-2035 | vdxo.contactevv@wisconsin.gov | Monday - Friday 7am-6pm

Agency's Sandata toll-free numbers: _____

Agency/Company ID: 2- _____

Worker Santrax ID: _____

Sandata Mobile Connect Username: _____

Client Identifier: _____

Service Code(s): _____

Is recording tasks within EVV required? Yes No

Service Code	SMC Service Code	TVV Service Code #
Personal and Supportive Care Services		
T1019	Personal Care Svc/15 min	10
S5125	Supportive Home Care/15 min	15
S5126	Supportive Home Care/Day	20
T1020	Personal Care/Day	25
Combo	Combo-PCS & SHC	30
99509	PCS Nurse Supervisory Visit/Visit	55
Home Health Care Therapy Services		
92507	Speech Therapy Individual/Visit	35
97139	Unspecified Therapeutic Procedure-OT/Visit	40
97799	Unspecified Rehab Svc-PT/Visit	45
Home Health Care Nursing Services		
99504	Mechanical Vent Care/Hour	50
S9123	Private Duty Nursing RN/Hour	65
S9124	Private Duty Nursing LPN/Hour	70
99800	Unspecified Home Visit-RN or LPN/Visit	60
T1001	Nursing Assessment or Eval/Visit	75
T1021	Home Health Aide or CAN/Visit	80
T1502	Med Admin-Oral, IM, Subq/Visit	85

P-02844A (10/2023)

www.dhs.wisconsin.gov/library/p-02844.htm

Kidokezo! Kitambulisho cha mfanyakazi ni mojawapo ya vidokezo bora tulivyo navyo kwa ajili yako. Kinapatikana kwenye tovuti ya DHS EVV ili kuchapisha na kujaza maelezo yanayohitajika na mfanyakazi. Mtoaji huduma atakuwa na maelezo haya yote. Tunaona jinsi kila sehemu itakavyotumika tunapoendelea leo.


Ikiwa ungependa kuunda nyenzo yako mwenyewe ili kuweka taarifa zako kwa urahisi (kama vile maelezo kwenye simu yako, au fomu tofauti iliyochapishwa), unaweza kutumia Kadi ya Ziara ya Wafanyakazi kutambua baadhi ya taarifa za msingi ambazo utahitaji kuwa nazo.

Kisanduku kilicho kwenye kona ya juu ya upande wa kulia ni msimbo wetu wa QR—njia ya mkato ya haraka ya kufikia Kitambulisho hiki kwenye ukurasa wetu wa tovuti. Fungua kamera kwenye simu yako ya mkononi, lenga kwenye kisanduku cha msimbo wa QR na usubiri kisanduku cha maandishi kijitokeze. Gusa kisanduku hicho kitakachojitokeza kwa kutumia kidole chako. Kitakupeleka moja kwa moja kwenye ukurasa huu wa tovuti.

Pia unaweza kutumia anwani ya tovuti iliyo chini ya slaidi.

Programu ya SMC

- EVV hutambulisha eneo mwanzoni na mwishoni mwa ziara. Haifuatili eneo kabla, baada, au wakati wa ziara.
- Chagua "Allow While Using App (Ruhusu Unapotumia Programu)."




Kama vile kwenye programu zingine, swali hili litajitokeza kwanza unapopakua programu: "Allow Sandata Mobile Connect to use Location? (Ruhusu Sandata Mobile Connect kutumia eneo lako?)" Tunapendekeza kuchagua chaguo la Ruhusu huku Unapotumia Programu hii.

Nitawapa nyote dakika moja ya kugusa kitufe cha Ruhusu huku Unapotumia Programu kwenye skrini hii.

Programu ya SMC

- Jina la mtumiaji: Weka anwani kamili ya barua pepe.
- Nenosiri: Weka nenosiri la muda mfupi kutoka kwa Sandata.
- Kitambulisho cha Kampuni: Chagua Kitambulisho cha kampuni yako kutoka kwa menyu ya orodha kunjuzi.



13

Mara ya kwanza unapoingia katika programu, hakikisha kuwa una Wi-Fi. Hii itahifadhi mipangilio yako. Programu hii inaweza kutumika bila Wi-Fi baada ya matumizi ya mpangilio huu wa kwanza.

Hii ni skrini ya kwanza ambapo utakuja kwanza utakapofungua programu. Itakufanya uingie kama “**Ambaye** anatoa huduma,” ambayo ni mojawapo ya pointi za data zinazohitajika tulizopitia. Endelea na utumie kidole chako kwenye slaidi hii huku tunapitia kila kipengee.

Jina lako loa mtumiaji: Kama tulivyoona tayari, jina lako la mtumiaji ni anwani ya barua pepe ambapo ulipokea barua pepe ya Sandata.

Nenosiri Lako: Mara ya kwanza unapoingia, tumia nenosiri la muda mfupi lililo katika barua pepe ya Sandata. Unaweza kunakili na kubandika kutoka kwenye barua pepe, au uweke kwa makini nenosiri hilo la muda mfupi hapa. Nenosiri hilo la muda mfupi ni la matumizi ya mara moja tu—utaombwa uweke upya nenosiri lako katika skrini chache zinazofuata.

Kidokezo! Tumia aikoni ya jicho kuona kile ulichoweka. Mshale wetu unaelekezwa kwake hapa.

Kitambulisho cha Kampuni: Programu inapotumiwa pamoja na Wi-Fi, sehemu hii itajaza kiotomatiki kwa orodha kunjuzi ya kila kampuni inayohusiana na mfanyakazi. Ikiwa mfanyakazi ako na mtoa huduma mmoja tu, mtoa huduma huyo mmoja ataonyesha kiotomatiki. Hii ni mojawapo ya maboresho ya programu. Wauguzi wa Kujitegemea, hii itaonyesha jina la biashara yako.

Juu tu ya kitufe cha Kuingia kuna chaguo la Nikumbuke. Hii itaweka jina lako la mtumiaji kiotomatiki katika siku zijazo. Bado utahitaji kuweka nenosiri lako kwa usalama bora.

Utaona picha ya skrini hapa kuwa simu hii ya mtumiaji ina chaguo la kuongeza Kitambulisho cha uso, chini tu ya kitufe cha "ingia" Hebu tuangalie sehemu inayofuata kwa mengi kuhusu hilo.

Machaguo na Mipangilio




WISCONSIN DEPARTMENT
of HEALTH SERVICES

Mara unapoingia kwa mara ya kwanza, kwa kutumia Wi-Fi, huenda ukataka kufikia baadhi ya vipengele mbalimbali ndani ya programu na ndani ya kifaa chako.

Machaguo ya Kugusa/Uso/Alama ya kidole

Kifaa chako kinaweza kuwa na mojawapo ya machaguo haya ya kuingia.



15


Baadhi ya vifaa hutoa machaguo ya Kugusa, Uso, au Alama ya kidole ya kuingia kando na nenosiri la kawaida. Huenda ukafuata vidokezo ili kuweka mojawapo ya machaguo haya kwenye kifaa chako.



Hakuna lolote kati ya haya linalohitajika.

Kuna urahisi unaotolewa na teknolojia ya simu, sio hasa na Sandata. Unalenga kufanya kuingia katika programu kuwa rahisi zaidi kwa kutumia maelezo yaliyohifadhiwa katika simu yako tu. Ukichagua kutumia teknolojia hizi, hutahitaji kuweka nenosiri lako kila wakati, lakini bado utahitajika kuweka upya nenosiri lako la Sandata mara kwa mara, kama kawaida.

Kwa mara nyingine tena, hii haihitajiki. Ni chaguo lako na unaweza kubadilisha mawazo yako baadaye katika Mipangilio ya programu yenyewe. Hivyo, unaendaje kwenye mipangilio? Hebu tuone! Endelea, Amber:

Mipangilio

Tumia 
Aikoni ya
menyu kwenye
upande wa
kushoto wa juu
ya kifaa chako.



16

Aikoni mbili zilizowekwa kwenye mstari kwenye upande wa kushoto wa juu wa skrini ya programu ni menyu yako. Kwa kuibofya—na kwa ajili ya kujifunza, endelea na uibofye kwenye skrini hii ya PowerPoint sasa— ufungue machaguo haya:

- Ziara—Huonyesha orodha ya ziara za hapo awali. Utaweza kuona ziara zote kutoka siku saba zilizopita. Hadi wakati huo, itaonyesha siku za mwisho tano.
- Wateja—Hufungua chaguo la kutafuta kwa mteja kuanza ziara.
- Mipangilio—Kama inavyoonekana hapa kwenye upande wa kulia, hii hukupa uwezo wa kubadilisha ni lugha gani ambayo programu inatumia kwa ajili yako kutoka kwa orodha ya machaguo 16. Pia unaweza:
 - Kubadilisha nenosisi lako.
 - Amua kutumia Kitambulisho cha kugusa ikiwa kifaa chako kina teknolojia hiyo (na kumbuka, bado unahitaji kubadilisha nenosiri lako mara kwa mara kama kawaida, lakini utaweza kutumia alama yako ya kidole kwa kuingia kwa kawaida).
 - Tazama ni nini ingine imewekwa kuwa "mipangilio ya wakala." Hii hufafanua jinsi ambavyo programu imewekwa na Wisconsin Department of Health Services (DHS) (Idara ya Huduma za Afya ya Wisconsin) Haziwezi kubadilishwa lakini hutoa maelezo kwa wale walio wadadisi.
- Usaidizi: Ikiwa uko kwenye mtandao, hii itakupeleka kwenye ukurasa wa tovuti wenye nyenzo za mafunzo za programu ya SMC ya Sandata Unaweza kuandika maneno ya kutafuta au kubofya kipengee kutoka orodha yao ya mada.

Hebu tuangalie kwa karibu chaguo maarufu, kinachofuata "Badilisha nenosiri". Endelea na uliguse kwenye skrini ya kulia ya juu.

Nenosiri la SMC

Muda wa nenosiri huisha kila baada ya siku 60. Wafanyakazi wanaweza kuweka upya nenosiri lao wenyewe kutoka kwa:

- Menyu ya mipangilio
- Skrini ya kuingia

Change Password

Current password

New password

Confirm new password

Requirements

- 12 or more characters
- Uppercase letter
- Lowercase letter
- Number
- Special character

Continue

17


Utaona hapa kwamba inaonyesha mahitaji ya nenosiri kwenye skrini ya kifaa chako na kuchunguza mahitaji. Hii ni skrini ambayo huonyesha ikiwa utachagua Badilisha Nenosiri kutoka kwa menu ya Mipangilio, au ikiwa unachagua Kubadilisha Nenosiri kabla ya kuingia.

Kwa ajili ya faragha, manenosiri ya programu ya SMC lazima yabadilishwe kila baada ya siku 60. Onyo ya jumbe wa kuisha kwa muda wa nenosiri itaanza kujitokeza siku 10 kabla ya muda kuisha. Unaweza kuibadilisha mara kwa mara ikiwa inahitajika.

Wafanyakazi uweka upya nenosiri lao wenyewe kwa urahisi kutoka kwa Menu ya mipangilio, kama ambavyo tumeona tu, au Skrini ya kuingia.

Nenosiri la SMC

Wafanyakazi wana majaribio tano ya kuweka nenosiri sahihi kabla ya maelezo haya kutokea.



18

Wakati mwingine, huenda ukahitaji kuweka upya nenosiri lako kwa kuwa ulilishau! Unaweza kubofya kila wakati kiungo cha weka upya nenosiri kwenye sehemu ya chini ya skrini ya kuingia.

Wafanyakazi wana majaribio matano ya kuweka nenosiri kwa usahihi. Inaweza kusaidia kutumia aikoni ya jicho iliyo kando ya nenosiri ili kuweza kuona kile unachoandika kila wakati.


Hiki hapa ni kidokezo: Ikiwa umejaribu mara kadhaa bila mafanikio, bofya **“Reset Password (Badilisha Nenosiri)”** kabla ya jaribio lako la tano. Hii ndio njia rahisi zaidi ya kuweka upya nenosiri na kuendelea.

Hata hivyo, baaada ya kuweka nenosiri lisilo sahihi mara ya tano, utapata ujumbe wa katikati unaokwambia uchague Reset Password (Kuweka Upya Nenosiri) kutokakwa skrini ya kuingia. Baada ya kujaribu mara nyingi sana bila kufanikiwa, utakuwa na hatua chache za kukamilisha. Utapata barua pepe ilio na mstari wa mada, "Sandata Mobile Connect Reset Password (Kuweka Upya nenosiri kwa Sandata Mobile Connect)," na utumie kiungo kuweka upya nenosiri lako. Njia hii ya kuweka upya huzuia **wakala wako wa EVV** au mtoa huduma kwa mteja kuhitaji kukusaidia. Ni kipengele kingine kipya katika programu hii mpya.

Kwa sote ambao tunajifunza kwa kufanya: Chukua kidole chako na uguse Weka upya Nenosiri kwenye slaidi hii. Kumbuka, njia rahisi zaidi ni kutumia chaguo hili kabla ya jaribio la tano.

Mipangilio ya Kifaa

Kwa utendakazi wa hali ya juu, hakikisha kuwa unapokea sasisho za programu.



19

Hebu tutazame baadhi ya mipangilio ambayo inaweza kuwa kwenye kifaa chako binafsi. Ya kwanza ni sasisho za programu.

Kama sheria ya kawaida, programu hufanya kazi vyema zaidi inaposasishwa mara kwa mara. Huduma yetu ya Mteja ya EVV imegundua kuwa baadhi ya matatizo ya programu husuluhishwa haraka wakati programu ya sasisho zote zimesakinishwa kwenye programu ya SMC. Programu isiyo na sasisho huenda ikaanza kuwa na hitilafu ya kiufundi. Unaweza kuzuia hilo!

Unaweza kufanya hivi kwa njia moja ya hizi mbili:

- Kwanza: Kupitia mipangilio yako maalum ya kifaa, chagua Sasisho Otomatiki. Hii hapa ni picha ya skrini ya jinsi hiyo inaweza kuonekana. Bila shaka, kila kifaa huwa tofauti, hivyo elewa kifaa chako na mipangilio yake.
- Pili: Futa na kisha usakinishe tena programu mara kwa mara. Sasisho za kila mwezi za programu ni za kawaida. Unaweza kuchagua ni mara ngapi ungependa kufuta na kusakinisha upya ili kunasa sasisho hizi. Hii haitabadilisha nenosiri la programu yako au mipangilio mingine.

Kumbuka - Mojawapo ya haya yatafanya kazi. Ni chaguo lako.

Mipangilio ya Kifaa

Kuwasha huduma za eneo za kuingia na kutoka kunahitajika.



20

Kidokezo chetu cha mwisho kuhusu mipangilio: Vifaa vitahitaji Huduma za Eneo kuwashwa. Hii inahitaji tu wakati wa kuingia na kutoka. Haifuatili eneo.

Kidokezo: Je, programu inaonekana kutojibu? Angalia mipangilio ya Huduma za Eneo lako ikiwa Huduma za Eneo lako zimewashwa, programu haitaendelea zaidi ya skrini ya kufunga.

Anza Ziara

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.




Hayo yalikuwa baadhi ya maelezo muhimu sana!

Hebu tutazame jinsi kuingia kwa ajili ya ziara kutaonekana mara programu na kifaa chako kitakapowekwa.

Kuanza Ziara

- Mara unapoingia, tafuta mteja kwa kuingia katika Kitambulishi chao cha Mteja (tarakimu sita) au Kitambulisho cha MA.
- Ikiwa mteja hawezi kupatika, ziara isiyojulikana inaweza kuanzishwa.



22

Baada ya kuingia katika programu, skrini ya mteja huyu itaonyeshwa.

Programu ya SMC hutumia kitambulishaji cha mteja cha tarakimu sita ili kumpata mteja au mshiriki. Hii inasimamia “**ni nani** anayepokea huduma” ya vipengele vinavyohitajika vya data kuu. Kitambulishaji cha mteja cha tarakimu sita kinaweza kupatikana kwenye Kitambulisho cha Mfanyakazi tulichorejelea hapo awali katika mafunzo.


Kwa sote ambao tunajifunza kwa kufanya: Chukua kidole chako na uguse eneo ambapo unaweka Kitambulisho cha mteja. Unataka akili yako na misuli zikumbuke kwa pamoja!

Ikiwa mteja hawezi kupatikana au Kitambulisho cha Mteja hakijulikani, unaweza kubonyeza kitufe cha Anzisha Ziara Isiyojulikana katikati mwa skrini. Wakati mwingine Ziara Isiyojulikana inaweza kuanzishwa wakati mojawapo ya masharti inatumika:

- Ustahiki wa mteja wa Medicaid hauko kwenye faili bado.
- Idhini bado haijatumwa kwa Sadanta au taarifa haijakamilika.
- Mfanyakazi hana Kitambulisho sahihi cha mteja.
- Hauko kwenye mtandao—maelezo zaidi kuhusu hilo baada ya muda mfupi.

Kuanza Ziara

- Mara mteja anapothibitishwa, bofya **Start Visit (Anza ziara)**.



23



Thibitisha maelezo ya mteja kwenye skrini kabla ya kuchagua Anza Ziara.

Chukua kidole chako na uguse Anza Ziara kwenye slaidi.

Gundua kwamba hapa kuna kipengele kipya: Ikiwa una huduma ya Wi-Fi, una chaguo la kupata maelekezo ya anwani ya mteja au umpigie simu. Rahisi!

Kuanza Ziara

- Chagua huduma inayotolewa.
- Bofya **Start Visit (Anza Ziara)**.



24

Huduma zinazotolewa zitahitaji kuchaguliwa baadaye. Hii hunasa “**ni huduma** gani inayotolewa,” ambayo ni nyingine ya pointi kuu za data. Tena, maelezo haya mtoaji huduma anaweza kuhakikisha kuwa yako kwenye Kitambulisho cha mfanyakazi tulichozungumzia hapo awali.



Wakati mwingi, unapaswa kuona machaguo tu yanayotumika kwa mteja huo maalumu. Kuanzia katikati ya Desemba 2023, wateja wa huduma za utunzaji wa afya wa nyumbani na misimbo yao ya huduma itapatikana.

Hakikisha kuwa maelezo ni sahihi—katika sampuli yetu, sampuli (sio halisi) jina la mteja ni “Jean Grey” na tunatoa huduma za usaidizi za utunzaji wa nyumbani. Hii ndiyo **ni nani, nini**, na **lini** ya pointi kuu za data. Ili Kuanza Ziara na kisha Ndiyo ikiwa maelezo yote ni sahihi.

Chukua kidole chako na uguse kitufe cha Ndiyo kwenye slaidi hii. Unataka akili yako na misuli zikumbuke kwa pamoja!

Kuanza Ziara

- Chagua Home (Nyumbani) au Community (Jamii).
- Bofya **Continue (Endelea)**.
- Bofya **Yes (Ndiyo)**.



Scrini hii inayofuata pia ni kipengele cha kufikia Desemba 2023.
Chagua Home (Nyumbani) au Community (Jamii) ambapo ziara inaanzia.


Mtoaji hudua wako anapaswa kukujulisha ikiwa kuna miongozo yoyote ya kufuata kuhusu kutoa huduma katika jamii.

Kisha bofya Endelea na Ndiyo ili kuanzisha ziara.

Endelea na ubofye maeneo hayo kwenye slaidi hii kwa kidole chako sasa. Nyumbani au Jamii, Endelea na kisha Ndiyo.

Kuanza Ziara

- **Visit in Progress (Ziara inaendelea)** itaonyeshwa juu.
- Wakati huu, programu ya SMC inaweza kufungwa.
- SMC hujifunga kiotomatiki baada ya dakika tano za kutotumika.



26

Sasa “Ziara Inaendelea” inaonyeshwa juu. Unaweza kuona wakati wa kuingia umeonyeshwa.

Chagua Home (Nyumbani) au Community (Jamii) ambapo ziara inaanzia.

Hakikisha umefikia skrini hii ya uthibitishaji kabla ya ubadilishe na kwenda kwenye programu zingine au kuweka chini simu yako, ili usipoteze maelezo uliyoweka. Ili kulinda faragha ya mteja/mshiriki, programu ya SMC hukuondoa ikiwa:

- Utapiga picha ya skrini, kupokea simu, au kufungua programu mpya kama vile muziki, vidokezo, au maandishi.
- Hujatumia programu ndani ya dakika tano.


Ni hivyo! Hivyo sasa unaweza kufunga programu: Programu haihitaji kuwa imefunguliwa wakati wa ziara halisi. Nenda tu kwenye aikoni ya menyu kwenye upande wa kushoto wa juu na uchague Kutoka. Endelea na uguse hiyo sasa kwenye skrini hii.

Kamilisha Ziara

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.

Kamilisha Ziara

- Ingia.
- Fungua aikoni ya menu na uchague Visits (Ziara).
- Tumia Kichupo upcoming (kinachokuja).
- Bofya ziara.



28


Utakapokuwa tayari kukamilisha ziara, ingia tena katika programu ya SMC. Fungua menu, kama ulivyokuwa ukifanya hapo awali.

Kuwa tayari kugusa skrini ninapoeleza hili:

- Chagua Ziara.
- Chagua Kichupo kinachokuja,
- Utaona maelezo ya mteja, ya ajabu, yenye wakati wa kuanza.
- Bofya kwenye kisanduku cha Ziara Inaendelea (buluu isiyokolea).

Kamilisha Ziara

- Chagua **Complete Visit (Kamilisha Ziara)**.
- Chagua Home (Nyumbani) au Community (Jamii).
- Bofya **Continue (Endelea)**.



29

Tuko katika skrini za mwisho za haraka sasa! Kwa kidole chako, gusa vitufe hivi kwenye slaidi hii:

- Chagua Kamilisha Ziara.
- Kama vile tu wakati wa kuanza kwako kwa ziara, utaombwa kuchagua Nyumbani au Jamii pa pale ulipo mwishoni mwa ziara. Kipengele hiki kipya kitaanza katikati ya Desemba 2023.
- Kisha chagua Endelea.

Kamilisha Ziara

- Bofya **Confirm** (Thibitisha).

9:55

Visit in Progress

Wonder Full

Service:
Unspecified Home Visit - RN and LPN/Visit
Switch Service
Clock In
09:30 AM

TASKS NOTES

Visit notes

Visit Summary ×

Wonder Full

Date
Thursday, September 7, 2023

Service:
Unspecified Home Visit - RN and LPN/Visit

Clock In Clock Out
9:30 AM 9:55 AM

Notes

Confirm

Na sasa—huku wakati wa kuondoka ukionyesha kwenye Muhtasari wa Ziara, bofya Thibitisha.

Ikiwa kuna marekebisho yoyote yanayohitajika ya wakati wako wa kuingia na wa kutoka, mjulishe msimamizi wako wa mtoa huduma. Wanaweza kufanya marekebisho kwenye Sandata Portal (Mtandao wa Sandata). (Kwa mfano, ulisahau kuondoka saa 10. asubuhi, lakini ghafla ukakumbuka saa 10:30. asubuhi na ukaondoka wakati huo).

Machaguo ya Kuondoka kwenye Ziara

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.



Sasa hebu tuzungumze kuhusu chaguo la kuondoka kwenye Ziara



Hautatumia chagua la kuondoka kwenye ziara mara kwa mara, lakini linaweza kusaidia. Hebu tuseme ninafanya kazi katika nyumba ya Martha, alkini nilisahau kuonyesha kuwa nimetoka kabla ya kuondoka. Baadaye nitakapofungua programu ya SMC—labda ninapojaribu kuingia kwa ziara mpya kwenye nyumba ya Scott—nitaiona skrini hii na kuona kuwa ziara yangu na Martha bado “inaendelea.” aha aha! Hapo ndipo ninapoweza kutumia Jiondoe kwenye Ziara. Hiyo itahakikisha kwamba ziara yangu na Martha imehifadhiwa na ninaweza kuanzisha ziara mpya na Scott. Pia nitahitaji kupigia wakala wa mtoa huduma wangu na kuwajulisha wakati ambapo kwa kweli nilitamatisha ziara yangu na Martha.

Kwa hivyo hii hutumika unaposahau kuondoka mwishoni mwa ziara. Inaweza kufanyika, hivyo tuangalie skrini hizo.

Machaguo ya Kuondoka kwenye Ziara

Aikoni ya Kopo la Taka

- Bofya Kopo la Taka katika kona ya kulia juu.
- Bofya **Yes (Ndiyo)** ili kujiondoa kwenye ziara.



32

Kunazo njia mbili za kujiondoa kwenye ziara.

Ya kwanza ni kwa kutumia aikoni ya taka katika kona ya juu ulia ya skrini. Mfano wetu hapa ni kutoka kwa ziara ya kikundi, lakini hii inaweza kufanyika katika ziara yoyote.



Kisha bofya Ndiyo ili kuthibitisha.

Endelea na uguse hizo zilizo kwenye slaidi hii sasa.

Machaguo ya Kuondoka kwenye Ziara

Katika Ziara

- Bofya Kitufe cha **Abandon Visit (Jiondoe kwenye ziara)**.
- Bofya **Yes (Ndiyo)** ili kujiondoa kwenye ziara.



Chaguo la pili, ikiwa uko katika ziara (katika mfano huu ziara ya kikundi), ni kutumia kitufe cha kujiondoa kwenye ziara. Tunao maraba wa rangi ya machungwa karibu nacho hapa. Kisha bofya ndiyo ili kutamatisha ziara.

Bofyo hiyo kwenye skrini ya slaidi hii.

Wakati Programu ya SMC haiko Mtandaoni.

Sasa Nini?


Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.



Hakuna Wi-Fi Hakuna tatizo! Programu ya SMC haihitaji Wi-Fi au huduma ya simu. Hebu tutazame jinsi ambayo hii hufanya kazi.

Modi ya bila Mtandao ya SMC

- Ziara zinaweza kuchukuliwa kwa kutumia programu ya SMC bila Wi-Fi au huduma ya simu; hii inaitwa Offline mode (Modi ya bila mtandao).
- Kibango cha **Offline (Nje ya mtandao)** kitaonyeshwa unapofanya kazi katika modi ya je ya mtandao.
- Ingia kama kawaida.



35

Ikiwa mfanyakazi hana ufikiaji wa Wi-Fi au huduma ya simu, ziara bado inaweza kunaswa kwa kutumia modi ya nje ya mtandao.

Unaweza kuona unapokuwa katika modi ya nje ya mtandao kwa sababu ya kibango kilicho juu.

Kidokezo: Ikiwa programu ninayopakua itaonyesha mviringo unaozunguka na kuzunguka na kamwe hauingii kwenye skrini hii ya kuingia, hii inamaanisha signali ya simu haiko imara vyakutosha kuandikisha, hivyo programu hiyo inaendelea kutafuta, kutafuta, kutafuta.


Suluhisho ni kwa "kuisaidia" programu kuamua ikiwa ina signali za kutosha kwa (1) kujaribu kuboresha signali—kwa mfano, kwenda kwenye dirisha au kti kwa signali bora zaidi au kutumia data ya simu ili kuongeza signali, au (2) kuweka simu ya rununu kuwa kwenye Modi ya Ndege ili kusiwe na signali na hivyo hitaji la ziara ya nje ya mtandao litakuwa wazi.

Ingia kama kawaida kwa kutumia jina la mtumiaji na nenosiri lako. Kisha, tunapofanya hivi na kubofya Ingia, tunaona slaidi inayofuata.

Modi ya bila Mtandao ya SMC

Sehemu ua Utafutaji ya Mteja haipatikani katika modi ya nje ya mtandao Kwa hivyo, mfanyakazi atahitaji kuanza ziara isiyojulikana.

- Sehemu ya Utafutaji ya Mteja huwa yenye rangi ya kijivu ikiwa katika modi ya Nje ya mtandao.
- Bofya **Start Unknown Visit (Anza Ziara Isiyojulikana)**.



Skrini hii ndipo ambapo ziara ni tofauti kiasi.

Katika ziara ya Nje ya mtandao, sehemu ya Utafutaji ya Mteja haipatikani—huwa yenye rangi ya kijivu. Chaguo lililobaki kwenye skrini ni Kuanza Ziara Isiyojulikana. Bofya kitufe hicho.

Modi ya bila Mtandao ya SMC

- Weka maelezo ya mteja.
- Bofya **Start Visit (Anza Ziara)**.
- Anza Ziara ya Kikundi haipatikani katika modi ya bila mtandao.
- Maelezo yatapatikana kwa mtoaji huduma wakati huo mwingine utakapoingia kwa huduma ya mtandao.

12:58 PM 90%

Start Unknown Visit X

Please enter the client's name to continue.

First Name
Ron

Last Name
Asch

Medicaid ID (optional)

Client ID (optional)
199272

Start Visit

Weka maelezo: Jina la kwanza na la mwisho la mteja.

Utaona eneo la kujaza Kitambulisho cha mteja. Kitambulisho cha Mteja ndiyo nambari bora ya kutumia. Ni nambari iliyopeanwa na Sandata ambayo mtoaji huduma anapaswa tayari kupeana kwa wafanyakazi. (Ikiwa una nambari nefu zaidi ya Kitambulisho cha Medicaid unaweza kuitumia badala yake)

Bofya Anza Ziara. Kama tulivyoona hapo awali, utaombwa kuthibitisha na utaona skrini ya Ziara Inaendelea. Mafanikio!


Hatua za kukamilisha ziara isiyojulikana ni sawa kama ambavyo tayari tumeonyeshwa.

Kidokezo cha haraka: Katika modi ya nje ya mtandao, Ziara haitaonyesha kwenye Sandata EVV Portal (Tovuti ya Sandata EVV) ambao msimamizi wako wa EVV hutumia hadi uingie katika programu ya SMC baadaye katika muunganisho wa mtandao. Maelezo hutumwa wakati huo. Hiyo inaweza kuwa siku iyo hiyo au wakati wowote ndani ya siku 7 zinazofuata. Iwapo unafanya kazi na wakala, tafadhali uliza ni muda gani wangependa uwasilishe katika huduma ya mtandao.

Usaidizi wa Mfanyakazi

Huduma ya Wateja ya Wisconsin EVV

- Simu: 833-931-2035
- Barua pepe: vdxc.contactevv@wisconsin.gov
- Jumatatu–Ijumaa: 7 asubuhi –6 jioni Saa za kati



Mara unapoanza kuitumia kuingia, huenda ukawa na maswali ya ziada. Ukifanya hivyo, tafadhali pigia huduma ya Mteja ya EVV. Wanapatikana ili kukusaidia kwa matatizo yoyote ya programu ya SMC ambayo huenda ukakumbana nayo. Wasiliana na Huduma kwa Wateja ya EVV ikiwa una maswali yoyote kuhusu rasilimali za mafunzo, EVV jimboni Wisconsin, ForwardHealth Portal (Mtandao wa Forwardhealth), au ikiwa una maswali kuhusu jinsi ya kutumia programu ya SMC.

Huduma kwa Wateja ya EVV inaweza kufikiwa kwa simu au barua pepe Jumatatu–Ijumaa 7 asubuhi hadi 6 jini. Saa za kati.

Msimbo wa QR ulio hapa utaleta nambari zao za simu ili uweze kuihifadhi kwenye orodha ya wasiliani ya simu yako.

Nyenzo za Mafunzo ya EVV



WISCONSIN DEPARTMENT OF HEALTH SERVICES

Home | About | Services | Training & Education | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support

Electronic Visit Verification (EVV): Training Workers

EVV Home

What's New

Members

FAQ

Resources

Phone

Alternate EVV

Training

Resources and FAQs

Contact Us

Stay connected
Join our email list

How questions? Need help?

Information workers will need to enter other they complete visits using EVV

Information workers will need to enter other they complete visits using EVV

Resource Title	Description	Language Available
General		
EVV Informational Video	Learn what EVV is and how EVV information is collected during a visit by watching this short video (2:30 minutes)	English
EVV Fundamentals-All Care User	A video to learn the purpose of EVV, the methods for verifying a client visit, steps needed to start implementing EVV, and when to file EVV resources. (28:54)	English
EVV Service and Visit List	Information workers will need to enter other they complete visits using EVV	English (PDF), Burmese (PDF), Spanish (PDF), Samoan (PDF), Tagalog (PDF), Vietnamese (PDF)
EVV Worker Visit Template	A card that workers can use along with to capture client information.	English
Mobile Visit Verification with the Sandata Mobile Connect app		
EVV Essentials: How to Use the SMC App	A video to learn everything needed to use the Sandata Mobile Connect app, also known as the SMC app. You'll also learn the steps needed to capture a client visit even when Wi-Fi or phone coverage is not available. (27:08 minutes)	English
Download the		

www.dhs.wisconsin.gov/evv/training-workers.htm

Kwa yeyote aliye mgeni kwenye jukumu la mfanyakazi la EVV au anayehitaji mafunzo tena kuhusu mchakato au mada maalumu ya EVV, kuna rasilimali nyingi za mafunzo.

Msimbo wa QR au kiungo kitakupeleka kwenye ukurasa wa rasilimali za Wafanyakazi wa Mafunzo ya DHS EVV. Utapata nyenzo unazoweza kuchapisha katika lugha ya Kiingereza, Kihispania, Hmong na lugha zingine, na pia video za mafunzo.

Chaguo Ioa Kubadilisha Huduma

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.



Sawasawa, sasa tunaenda kwenye salidi ambayo haitumiki na wauguzi wa kujitegemea, lakini inaweza tumika na wengine.


Hii ni kipengele ambacho kinaweza kuokolea muda kwa wengine wenyu.

Kumbuka, “huduma” ni aina hizi pana za utunzaji. Kumbuka, “huduma” inarejelea aina pana ya utunzaji unaotoa. Sio kazi zile ndogo, za kibinafsi (kama vile kusaidia kuvaa nguo au kupiga mswaki, kwa mfano) zinazofanywa wakati wa ziara na kukusanywa kwa rekodi ya utunzaji.

Hebu tupitie chaguo la Kubadilisha Huduma.

Chaguo la Kubadilisha Huduma

- Fungua aikoni ya menyu na uchague Ziara.
- Tumia Kichupo kinachokuja.
- Bofya ziara.
- Bofya **Switch Services (Badilisha Huduma)**.



41

Baadhi yenu huenda ikawa mnafahamu msimbo wa huduma ya Combo unaotumika katika IRIS (Iclude, Respect, I Self Direct) (IRIS (Jumuisha, Heshimu, Najielekeza Mwenyewe)). Wafanyakazi wa IRIS wanaotumia Sandata bado hutumia msimbo wa Combo wakati utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa usaidizi umeunganishwa. Huduma hii mpya ya Kubadilisha Huduma hutoa chaguo bora kwa kila mmoja.

Ni chaguo la ajabu, kwa kweli na hivyo tuna jina la mteja ambalo ni Wonder Full. If unabadilisha kutoka kwa aiana moja ya huduma (hapa, ziara ya nyumbani ya muuguzi aliyesajiliwa [RN] au muuguzi mtendaji aliyesajiliwa [LPN]) hadi kwa aina nyingine ya huduma katikati mwa ziara, hii ni njia rahisi ya kufanya hivi bila kuanzia mwanzo kwa huduma mpya.

Fungua menyu na uende kwenye Kichupo kinachokuja ili kuchagua—hatua zote tulizofanya hapo awali. Sasa tafuta Badilisha Huduma chini ya jina la mteja. Bofya Badilisha Huduma. Endeleva na ufanye hivyo sasa kwa nkidole chako kwenye skrini.

Chaguo la Kubadilisha Huduma

8:17

ALTERNATE LOCATION

Please select your location *

Home ✓

Community

CONTINUE

CANCEL

8:17

SERVICE SELECTION

Friday, August 4, 2023

MOUNT THOMAS

Please select the service you are providing

Unspecified Therapeutic Procedure - OT/Visit

Med Admin - Oral, IM, SUBQ/Visit ✓



START VISIT

42

Weka kidole chako tayari! Hii hapa ni utakayobofya baadaye:

- Unapobadilisha huduma, utaombwa kuchagua Nyumbani au Jamii kwa huduma uliyotamatisha.
- Chagua eneo la ziara ambapo huduma ilitamatishwa.
- Bofya Endelea.
- Kisha chagua aina mpya ya huduma (katika mfano wetu, huduma ya chini itachaguliwa) na uanze ziara.


Chaguo Ioa Kubadilisha Huduma



43

Kama kawaida, utaombwa kuchagua eneo la ziara ambapo huduma ya pili inaanzia. Kisha chagua Ndiyo ili Kuanza Ziara.

Chaguo loa Kubadilisha Huduma



44

Mafanikio! Skrini ya Ziara Inaendelea huonyeshwa! Kama kawaida, unaweza kuondoka kutoka kwa programu huku ukitoa huduma. Bofya kwenye aikoni ya mlango kwenye upande wa kulia juu na ubofye Toka.

Unaweza kubadilisha huduma mara kwa mara inavyohitajika na kutamatisha ziara nzima kama kawaida.


Chaguo la Ziara ya Kikundi

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

Ziara ya kikundi humruhusu mfanyakazi mmoja kutoa huduma katika mpangilio wa kikundi kwa wateja wengi bila kuingia na kuondoka kwa kila mmoja wao:

- Weka maelezo ya kwanza ya mteja kama kawaida.
- Gusa **Start Group Visit (Anzisha Ziara ya Kikundi)**.



46

Mtoaji huduma wako atakwambia ikiwa unaweza kutumia ziara ya kikundi. Ikiwa unatoa huduma kwa wateja wengi katika ziara moja katika eneo sawa na wana mlipaji na mtoaji huduma sawa wa programu, unaweza kuanza Ziara ya Kikundi.

Anza tu jinsi ambavyo ungeanza ziara nyingine yeyote: Ingia na uweke maelezo ya kwanza ya mteja. Skrini hii ni ambapo ungechagua Anza Ziara ya Kikundi.

Hii hukupa msingi wa ziara wa kuongeza wateja zaidi.

Kumbuka changuo la mwisho kwenye skrini, Join Group Visit (Jiunge na Ziara ya Kikundi), iliyoonyeshwa hapa na rangi ya machungwa X haitumiki Wisconsin kunasa ziara za EVV.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

- Chagua aina ya Huduma na ubofye **Continue (Endelea)**.
- Chagua Eneo na ubofye **Continue (Endelea)**.

The image displays two screenshots of a mobile application interface. The left screenshot shows a 'Select a Service' screen with a list of service options and a 'Continue' button at the bottom. The right screenshot shows a 'Select a Location' screen with 'Home' and 'Community' options and a 'Continue' button at the bottom.

Select a Service

- Mechanical Vent Care/Hour
- PCS Nurse Supervisory Visit/Visit
- Unspecified Home Visit - RN and LPN/Visit
- COMBO - PCS & SHC
- Supportive Home Care/15min
- Supportive Home Care/Day
- Private Duty Nursing - RN/Hour
- Private Duty Nursing - LPN/Hour
- Nursing Assessment or Eval/Visit
- Personal Care Svc/15min
- Personal Care/Day
- Home Health Aide or CNA/Visit
- Med Admin - Oral, IM, SUBQ/Visit

Select a Location

- Home
- Community



47

Baada ya kuanzisha Ziara ya Kikundi, utaombwa Kuchagua Huduma Chagua aina ya huduma na ubofye **Endelea**.

Kisha utahitaji kuchagua eneo, Nyumbani au Jamii, na ubofye **Endelea**.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

- Bofya **Yes (Ndiyo)** ili kuanza ziara ya kikundi.




Kinachofuata, utabofya Ndiyo ili kuanza ziara ya kikundi.

Kisha utaiona skrini unayoifahamu kwenye upande wa kulia, ikionyesha kuwa mteja wa kwanza amewekwa.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

- Kwa kutumia menyu, nenda kwenye Visits (ziara).
- Chagua kichupo Upcoming (Kinachokuja).
- Bofya Visit in Progress (Ziara Inaendelea).





Ili kuendelea, unahitaji kutumia msingi huo kama msingi wako:

- Katika Menyu, nenda kwenye Ziara.
- Chaguo kichupo kinachokuja. Utaona ziara hiyo ya msingi ambayo uliweka kwanza.
- Bofya kwenye ziara hiyo inayoendelea ili kuifungua.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

- Chagua **Add Client (Ongeza Mteja)**.
- Andika katika Kitambulisho cha Medicaid cha mteja anayefuata.
- Chagua **Start Group Visit (Anza Ziara ya Kikundi)**.
- Chagua msimbo wa huduma na eneo la mteja, kama kawaida.
- Rudia kwa wateja wengine.



50

Kutoka pale, unaweza kuongeza wateja mmoja baada ya mwingine:

- Chagua Ongeza Mteja.
- Andika katika Kitambulisho cha Medicaid cha mteja anayefuata, kama kawaida.
- Chagua Anza Ziara ya Kikundi.



Skrini tayari zilikuwa zinafahamu, kuongeza huduma na eneo (nyumbani au jamii), will be itaonyeshwa badaye.

Unaweza kuendelea kurudi kwenye ziara katika menyu ili kuongeza wateja wengi inavyohitajika. Wateja wapya wanaweza kuongezwa wakati wowote wakati wa ziara.

Chaguo la Ziara ya Kikundi

Kutamatisha ziara ya kikundi kunaweza kufanyika mteja mmoja baada ya mwingine au kama kikundi kizima:

- Bofya ziara.
- Chagua **Resume Visit (Rejea kwenye Ziara)** kwa mteja mmoja baada ya mwingine **Complete Group Visit (Kamilisha Ziara ya Kikundi)** kwa wateja wote.



51

Kutamatisha ziara ya kikundi kunaweza kufanyika moja kwa moja au zote kwa pamoja. Huanza tu kama ambavyo ungetarajia:

Kutoka kwa menu, chagua Ziara na Kichupo kinachokuja. Bofya ziara. Kila mteja ataonyeshwa.

Ili kutamatisha ziara mteja mmoja baada ya mwingine:

- Rejea kwenye Ziara humaanisha utanza tena kukusanya data ya mwisho ya mteja huyu.
- Kuondoka kwenye ziara hughairisha ziara hiyo ya mteja. Utahitaji kumjulisha msimamizi wako wa wakala wa mtoaji huduma, ili aweze kufanya marekebisho katika Sandata Portal (mtandao wa Sandata).

Ili kutamatisha ziara zote za wateja kwa wakati mmoja, chagua Kamilisha Ziara ya Kikundi kwenye sehemu ya chini ya skrini.

Kwa njia yoyote, unaweza kutarajia skrini sawa unazozifahamu kama vile kiukamilisha yoyote ile.

Chaguo la Kazi na Vidokezo

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.



Baadhi ya watoaji huduma wanatumia EVV kukusanya rekodi ya maelezo ya utunzaji. Kwenye Kitambulisho cha Mfanyakazi, mtoa huduma anaweza kuorodhesha ikiwa kazi na vidokezo vinahitajika katika EVV au la.

Ikiwa hili ni jambo unalopaswa kufanya, liko kwenye skrini chache fupi mwishoni mwa ziara. Hebu tutazame.

Ikiwa mtoaji huduma wako haihitaji, hupaswi kuwa na wasiwasi kuhusu chaguo hizi.

Chaguo la Kazi na Vidokezo

Unapokamilisha ziara:

- Chagua kichupo cha Kazi.
- Bofya **Add Tasks (Ongeza Kazi)**.
- Chagua kutoka kwa orodha.
- Bofya **Done (Imekamilika)**.

Visit in Progress

Jessica Faucett

Service
HHO Physical Therapy
Switch Service

Clock In
10:24 AM

TASKS NOTES

Add Tasks

Complete Visit

Add Tasks

Assist Dressing Changing

Assist with Medication

Bathing

Eating Assistance

Errand

Grooming

Housekeeping

Laundry as needed

Done

53

Utagundua skrini hii kama mojawapo ya skrini za mwisho wakati wa mchakato wa kuondoka. Unaweza kuona Ziara Inaendelea kwenye sehemu ya juu na chaguo la Kukamilisha Ziara kwenye sehemu ya chini.

Kwenye skrini hii, ikiwa unahitajika kuweka kazi na vidokezo:

- nenda kwenye Kichupo cha kazi.
- Gusa Ongeza Kazi. Hiyo itafungua orodha sawa na ile unayoona kwenye upande wa kulia.
- Chagua kazi zote zinazofanywa wakati wa ziara kwenye orodha
- Chagua Imekamilika.

Chaguo la Kazi na Vidokezo

- Thibitisha kila kazi kwa kubofya mviringo wake.
- Chagua Kichupo cha vidokezo ikiwa inahitajika.
- Ongeza vidokezo.
- Gusa **Complete Visit (Kamilisha Ziara)**.



Visit in Progress

Jessica Faucett

Service
HHO Physical Therapy
Switch Service

Clock In
10:24 AM

TASKS NOTES

Add Tasks

Assist with Medication Clear

Task Completed

Complete Visit

54

Kinachofuata, utahitaji kuthibitisha kila kazi kwa kugusa mviringo ulio kando yake. Hii husaidia kuzuia hitilafu.

Ikiwa una vidokezo vya kuongeza, unaweza kuviweka kando katika kichupo cha Vidokezo.

Kutoka hapa, uko tayari kuchagua Kamilisha Ziara na ukamilishe ziara kama kawaida.

Chaguo la Uthibitishaji wa Mteja

Kanusho: Maelezo yote ya wateja yaliundwa kwa ajili ya mafunzo tu.



Hii ni kwa ajili ya watoaji huduma wanaotumia EVV kukusanya rekodi ya maelezo ya utunzaji. Ikiwa mtoaji huduma wako anahitaji kazi na vidokezo viko katika EVV, watahitaji pia mteja kuthibitisha.



Ikiwa hili ni jambo unalopaswa kufanya, liko kwenye skrini chache fupi mwishoni mwa ziara. Hebu tutazame.

Ikiwa mtoaji huduma wako haihitaji, unaweza kuchagua vitufe vya Skip (Ruka) kwenye skrini hizi zote.

Chaguo la Uthibitishaji wa Mteja

Baada ya mfanyakazi kuweka maelezo ya kuondoka:

- Bofya **Continue (Endelea)**.
- Pitisha kifaa kwa mteja.
- Chagua lugha.
- Bofya **Continue (Endelea)**.



56

Kila ziara itaonyesha skrini hii mwishoni. Kama kumbusho, ikiwa mwajiri wako hahitaji kazi, vidokezo na uthibitishaji wa mteja kwa EVV, unaweza kuchagua Kuruka hapa.

Ikiwa unahitajika kukusanya kazi, vidokezo na uthibitishaji wa mteja kwa kutumia EVV:

- Chagua Endelea.
- Pitisha kifaa kwa mteja ili aweke maelezo yake, ukianza kwa lugha wanayopendelea.
- Bofya Endelea.

Chaguo la Uthibitishaji wa Mteja

- Bofya **Confirm (Thibitisha)** au **Deny (Kataa)** kwa kila kipengee.
- Bofya **Continue (Endelea)**.
- Chagua Sahihi au Kurekodi Sauti.

Hello, Harriet
Please verify the details for today's visit.

Services

RN Assessment (T1001)
55 minutes
Confirm Deny

Specialized Skill Development (1:3)
1 hour, 7 minutes
Confirm Deny

Visit Time
10:02 AM - 12:05 PM
2 hours, 3 minutes
Confirm Deny

Continue

←
Sign or Record

SIGNATURE VOICE RECORDING

Use your finger to sign below.

Clear

Continue


57

Kwa kila kipengee kilichoorodheshwa, mteja anapaswa kubofya Thibitisha au Kataa na kisha kubofya Endelea.

Hii italeta skrini inayofuata. Mteja anaweza kutumia sahihi yake kuthibitisha (iliyoonyeshwa hapa), au kwenye slaidi—

Chaguo la Uthibitishaji wa Mteja

- Kwa kurekodi sauti, fuata vidokezo vilivyo kwenye skrini.



58


—Tumia kurekodi kwa sauti kwa jina lake na tarehe kama thibitisho.

- Ili kuanza kurekodi sauti, bofya mviringo wa rangi ya buluu.
- Ili kutamatisha kurekodi sauti, bofya mraba mwekundu.
- Bofya endelea utakapokamilisha.

Kumbuka, **ikiwa** mtoaji huduma wako anahitaji maelezo haya, unaweza kutumia chaguo la sauti au sahihi. Ikiwa mtoaji huduma wako hatahitaji uthibitishaji wa mteja, sehemu hii hurukwa.

Chaguo la Uthibitishaji wa Mteja

- Bofya **Done (Imekamilika)**.
- Mpatie simu mfanyakazi tena.



Hatua hizo chache ndizo zinazohitajika. Tena, mtoa huduma wako hahitaji uthibitishaji wa mteja, huhitaji kutumia skrini hizi.

Usaidizi wa Mfanyakazi




WISCONSIN DEPARTMENT
of HEALTH SERVICES

Usaidizi wa Mfanyakazi

Huduma ya Wateja ya Wisconsin EVV

- Simu: 833-931-2035
- Barua pepe: vdxcontactevv@wisconsin.gov
- Jumatatu–Ijumaa: 7 asubuhi –6 jioni Saa za kati



Mara unapoanza kuitumia kuingia, huenda ukawa na maswali ya ziada. Ukifanya hivyo, tafadhali pigia huduma ya Mteja ya EVV. Wanapatikana ili kukusaidia kwa matatizo yoyote ya programu ya SMC ambayo huenda ukakumbana nayo. Wasiliana na Huduma kwa Wateja ya EVV ikiwa una maswali yoyote kuhusu rasilimali za mafunzo, EVV jimboni Wisconsin, ForwardHealth Portal (Mtandao wa Forwardhealth), au ikiwa una maswali kuhusu jinsi ya kutumia programu ya SMC.

Huduma kwa Wateja ya EVV inaweza kufikiwa kwa simu au barua pepe Jumatatu–Ijumaa 7 asubuhi hadi 6 jini. Saa za kati.

Msimbo wa QR ulio hapa utaleta nambari zao za simu ili uweze kuihifadhi kwenye orodha ya wasiliani ya simu yako.

Nyenzo za Mafunzo ya EVV



WISCONSIN DEPARTMENT OF HEALTH SERVICES

Home | About | Services | Training & Education | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support | Health Care & Support

Home | Services & Resources | Electronic Visit Verification (EVV) Training Workers

Electronic Visit Verification (EVV): Training Workers

Train the workers who will use an EVV system to check in and out for visits. Use the combination of resources that makes the most sense for your agency and worker needs. Most workers will need to view all the resources. These resources can also be used as review and reference materials.

Refer to [Training Modules for Electronic Visit Verification](#) for training plan suggestions. As a reminder, training resources do not supersede DHS policy. Refer to [EVV Implementation and Support](#) for EVV policy information.

Additional languages for written materials can be requested at education@dhss.wisconsin.gov or 833-838-2033. Please allow 30 business days for translation and delivery.

Resource Title	Description	Language Available
General		
EVV Informational Video	Learn what EVV is and how EVV information is collected during a visit by watching this short video (2:58 minutes).	English
EVV Implementation Overview	A video to learn the purpose of EVV, the methods for verifying a client visit, steps needed to start implementing EVV, and when to call EVV resources. (28:34)	English
EVV Service and Visit List	Information workers will need to enter when they complete visits using EVV.	English (PDF), Burmese (PDF), Spanish (PDF), Samoan (PDF), Tagalog (PDF), Vietnamese (PDF)
EVV Worker Visit Template	A card that workers can use along with the schedule client information.	English
Mobile Visit Verification with the Sandata Mobile Connect app		
EVV Overview: How to Use the SMC App	A video to learn everything needed to use the Sandata Mobile Connect app, also known as the SMC app. You'll also learn the steps needed to capture a client visit even when Wi-Fi or phone coverage is not available. (21:08 minutes)	English
Download the		

www.dhs.wisconsin.gov/evv/training-workers.htm

Kwa yeyote aliye mgeni kwenye jukumu la mfanyakazi la EVV au anayehitaji mafunzo tena kuhusu mchakato au mada maalumu ya EVV, kuna rasilimali nyingi za mafunzo.

Msimbo wa QR au kiungo kitakupeleka kwenye ukurasa wa rasilimali za Wafanyakazi wa Mafunzo ya DHS EVV. Utapata nyenzo unazoweza kuchapisha katika lugha ya Kiingereza, Kihispania, Hmong na lugha zingine, na pia video za mafunzo.

Asante

Tafadhali shiriki maoni yako
kuhusu kipindi cha leo katika utafiti mfupi.



WISCONSIN DEPARTMENT
of HEALTH SERVICES

Programu ya SMC

▪ Chagua Lugha

Select Language
Please select your preferred language.

English

Español

русский

中国人

Soomaali

اللغة العربية

Continue

Confirm Language
Please confirm that you would like to select English as your language.

Confirm

Cancel

64

Huenda ukataka kuweka lugha nyingine kando na Kiingereza. Ili kufika pale, kwanza utaombwa kuchagua lugha unaoipendelea kutoka kwa orodha.

Kisha ni wakati wa kuweka nenosiri lako mpya na kubofya wasilisha. Utarudishwa kwenye skrini ya kuingia.

Lugha zinazopatikana: Kiingereza, Kiarabu cha Misri, Kiburma, Kichina cha Mandarin, Kifaransa, Kiindi, Hmong, Kilaoti, Kinepali, Kirusi, Kiserbia, Kisomali, Kihispania, Swahili, Kivietinamu